**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**DAR ES SALAAM**

**MAOMBI YA MAREJEO NA. 86 YA 2021**

**KATI YA**

**COSMAS YOHANA KARADIS.......................................... MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**COTEX INDUSTRIES LIMITED...................................... MJIBU MAOMBI**

Labour Court Tz.

**UAMUZI MDOGO**

*Tarehe ya Amri ya Mwisho: 28/09/2021*

*Tarehe ya Uamuzi: 12/11/2021*

**I. Arufani, J.**

Huu ni uamuzi unaotokana na pingamizi la awali (hapa utajulikana kama pingamizi) lililowasilishwa na mjibu maombi katika mahakama hii akieleza kwamba, maombi haya ya marejeo yaliyoko mbele ya mahakama hii yamewasilishwa katika mahakama hii nje ya muda.

Wakati wa kusikiliza pingamizi hili mjibu maombi aliwakilishwa na Wakili Paschal Mshanga, wakati mleta maombi aliwakilishwa na Bwana Sammy Katerega, Mwakilishi Binafsi. Wakili Mshanga aliieleza mahakama kwamba ni matakwa ya kisheria katika fungu la 91 (1) (a) la Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366 kama ilivyorejewa mwaka 2019 kwamba, maombi ya marejeo ya tuzo toka tume

yanapaswa yafunguliwe mahakama kuu ndani ya wiki sita tangu tuzo hiyo ilipowasilishwa kwa mteja. Alieleza kumbukumbu zinaonyesha kwamba mleta maombi alipokea nakala ya tuzo toka tume kupitia muwakilishi wake aitwaye Nehemia Munga mnamo tarehe 22/01/2021. Alisema ukihesabu kuanzia tarehe hiyo ya kupokea tuzo wiki sita zinaishia tarehe 05/03/2021. Alesema maombi haya yalifunguliwa mahakamani mnamo tarehe 09/03/2021 ikiwa zimepita siku nne (4) tangu tarehe ya mwisho kuwasilisha maombi haya. Akaeleza kuwa mleta maombi hakuomba ridhaa yoyote ya mahakama kuleta maombi haya nje ya muda.

Ilielezwa zaidi na Wakili wa mjibu maombi kuwa, ni kanuni ya kisheria kuwa shauri lolote linalofunguliwa nje ya muda linatakiwa kufutwa bila ruhusa ya kulirejesha tena mahakamani, alielekeza mahakama kwenye shauri la **Tanesco v. Bakari Mayombo** [2015] LCCD ambapo Mhe. Aboud, J. alitumia kanuni ya 55 (1) ya Kanuni za Mahakama ya Kazi na kifungu cha 3 (1) cha Sheria ya Ukomo wa muda kufutilia mbali shauri hilo. Kutilia msisitizo msimamo huo, Wakili Mshanga alirejea shauri la **Barclays Bank Tanzania Ltd. v. Phylisiah Hussein Mcheni**, Civil Appeal No. 19/2016. Wakili Mshanga alimalizia kwa kuiomba mahakama hii kufutilia mbali

Labour Court TZ.

maombi haya bila ruhusa ya kuyarejesha tena mahakamani kwa sababu, yaliwasilishwa mhakamani nje ya muda uliyowekwa kisheria bila ya ridhaa ya Mahakama.

Akijibu hoja za pingamizi hilo, Bwana Katerega alieleza kuwa, maombi haya yalifunguliwa ndani ya muda unaotakiwa kisheria na kupokelewa na mahakama hii tarehe 04/03/2021. Alisema hiyo inathibitishwa kwa nakala alizozipokea kutoka katika mahakama hii na nakala hizo zilipelekwa kwa Naibu Msajili tarehe 06/03/2021. Alieleza zaidi kuwa walipewa taarifa kuwa nyaraka zimepokelewa hivyo walete nyaraka halisi zilizopokelewa na kugongwa muhuri tarehe 09/03/2021.

Bwana kateregа aliendelea kueleza kwamba, bahati mbaya ni kwamba hakuna utaratibu uliowekwa na mahakama kuwa baada ya kupokelewa nakala hizo za maombi zinagongwa muhuri wa tarehe gani. Kwamba, kwa mujibu wa kanuni ya 8 (1) (c) ya Kanuni za Mahakama ya kazi, inaruhusu kuwasilisha maombi kwa njia ya barua pepe kwa Naibu Msajili na inaonekana wazi ni tarehe ipi inachukuliwa kuwa ni tarehe ya kupokea maombi. Maombi yakipokelewa kwa njia ya barua pepe hiyo ndiyo inachukuliwa kuwa ni tarehe ambayo maombi yalipokelewa mahakamani.

Labour Court Tz.

Bwana Katerega alimalizia kwa kuiomba Mahakama izingatie nyaraka zilizotolewa mahakamani, na kuruhusu maombi haya yaendelee kusikilizwa ili mleta maombi asiadhibiwe kwa kosa ambalo si la kwake.

Katika mawasilisho ya nyongeza, mjibu maombi alieleza kwamba nyaraka iliyotolewa na muwakilishi wa mleta maombi kuonyesha kuwa maombi haya yaliwasilishwa kwa njia ya barua pepe haiaminikii kutokana na kutoonyesha ni wapi alikoipata. Pia alipaswa ku wapatia nyaraka hiyo wakati alipowasilisha nyaraka za maombi lakini kaileta baada ya pingamizi kutolewa mahakamani.

Zaidi alieleza kwamba, hata kama nyaraka hiyo itazingatiwa bado inaonyesha kwamba shauri hili liliwasilishwa tarehe 06/03/2021 ambayo bado ni nje ya muda. Kwamba kwa mujibu wa waraka namba 148 wa mwaka 2018 tarehe ya kupokea shauri ni ile ya kuwasilisha shauri mahakamani. Pia Bwana Katerega hajaeleza ni barua pepe gani aliyoitumia kwa Naibu Msajili ili kuwasilisha maombi hayo. Wakili Mshanga alisisitiza wapewe nafuu alizoziomba katika mawasilisho yake ya awali.

Labour Court TZ.

Baada ya kutafakari kwa kina mawasilisho ya kutoka pande zote mbili kuhusu pingamizi la awali lilowasilishwa na mjibu maobi katika shauri hili mahakama imeona kwamba, kama ilivyo wasilishwa na wakili wa mjibu maombi, maombi ya marejeo ya uamuzi wa tume yanapaswa kufunguliwa katika mahakama hii ndani ya wiki sita toka tarehe ambayo tuzo imepokelewa na mdaawa kama ilivyoainishwa katika fungu la 91 (1) (a) la Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, na kusisitizwa na Mahakama ya Rufani katika shauri la **Serengeti Breweries Ltd. v. Joseph Boniface,** Civil Appeal No. 150/2015 CAT (Unreported).

Katika kumbukumbu za shauri hili, ni wazi kuwa mleta maombi alipokea Nakala ya tuzo tarehe 22/01/2021 hivyo alipaswa kuwasilishwa maombi yake ya marejeo katika mahakamani hii si zaidi ya tarehe 05/03/2021. Baada ya Mahakama kupitia nyaraka za shauri hili hasa nyaraka ambayo iliwasilishwa mahakamani na mwakilishi wa mleta maombi ili kuthibitisha kuwa maombi haya yaliwasilishwa ndani ya muda, imeona kwamba kupitia nyaraka hiyo maombi haya yaliwasilishwa mahakamani kwa njia ya mtandao tarehe 06/03/2021 saa 02:32:12 asubuhi na sio tarehe 04/03/2021 kama alivyoeleza mwakilishi wa mwombaji. Aidha aliwasilisha nakala ngumu za maombi

Labour Court Tz.

hayo katika masjala ya mahakama hii tarehe 09/03/2021 kama ilivyo utaratibu.

Mahakama ya Tanzania inatambua njia ya mtandao kama moja ya njia za kufungua shauri mahakamani. Kanuni ya 21 (1) ya Sheria ya **Judicature and Application of Laws (Electronic filling) Rules, 2018** inaeleza kwamba, nyaraka inatambulika kuwa imekwisha sajiliwa pale inapokuwa imewasilishwa kwa njia ya kieletroniki. Kwa ufafanuzi zaidi kanuni hiyo inaeleza kama ifuatavyo:-

> *'A document shall be considered to have been filed if it is submitted through the electronic filing system before midnight, East African time, on the date it is submitted, unless specific time is set by the court or it is rejected.'*

Bwana Katerega ameeleza katika mawasilisho yake kuwa, maombi haya yalifunguliwa ndani ya muda yaani tarehe 04/03/2021. Kama ilivyolezwa na wakili wa mjibu maombi maelezo yake sio sahihi kwa kuwa nyaraka aliyoileta mahakamani kuthibitisha kufungua shauri hili kwa njia ya kieletroniki inaonyesha kuwa maombi haya ya marejeo namba 86 ya mwaka 2021 yalifunguliwa tarehe 06/03/2021 na sio tarehe 04/03/2021 kama alivyowasilisha mwakilishi wa mleta maombi.

Labour Court Tz.

Kwa msingi huo ni wazi kuwa maombi haya yaliwasilishwa mahakamani nje ya muda kwa kuchelewa kwa siku moja. Na mleta maombi hakuomba ruhusa ya mahakama kuwasilisha maombi yake nje ya muda. Pamoja ni kuwa mleta maombi alichelewa kwa siku moja kuwasilisha maombi yake katika mahakama lakini kama ilivyoelezwa na Mahakama ya Rufani katika shauri la **Wambele Mtumwa Shaban V. Mohamed Hamis**, Civil Reference No. 08 of 2016 mahakama zetu zimekuwa zikisisitiza kwamba kuchelewa hata kwa siku moja ni kuchelewa (*delay of even a single day is a delay*).

Hivyo maombi haya yanaonekana hayako mahakamani kwa usahihi kwa sababu yalifunguliwa mahakamani nje ya muda uliowekwa kisheria bila ya ridhaa ya mahakama. Kwa maelezo hayo ni kwamba pingamizi la mjibu maombi linakubaliwa na maombi haya yanafutiliwa mbali kwa kuwasilishwa mahakamani nje ya muda unaotakiwa kisheria. Imeamriwa hivyo.

Imewekwa saini hapa Dar es Salaam leo tarehe 12 ya Mwezi Novemba, 2021.

I. Arufani
**JAJI**
12/11/2021

Labour Court Tz.

**<u>Mahakama</u>**: Uamuzi mdogo umesomwa leo tarehe 12 mwezi wa Novemba, 2021 akiwepo Bw. Sammy Katerega, Mwakilishi wa Mleta Maombi na akiwepo Bw. Paschal Mshanga, Wakili wa Mjibu Maombi. Haki ya kukata rufaa kwenda Mahakama ya Rufani imeelezwa.

I. Arufani
**<u>JAJI</u>**
12/11/2021

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA (The High Court of Tanzania) (Labour Division) DIVISHENI YA MAHAKAMA YA KAZI

Labour Court Tz.